**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA NNE WA BUNGE LA 13 JIJINI DODOMA TAREHE 04 SEPTEMBA, 2026**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia hatua hii tukiwa na afya njema na uzima, na tukiwa tunahitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano wa Nne wa Bunge la 13.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** mbele ya Bunge lako tukufu, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza vyema na kwa juhudi zake za kuwatumikia wananchi wa Tanzania. Sisi sote ni mashahidi na tunaona jinsi anavyofanya kazi bila kuchoka katika kuleta maendeleo kwa taifa hili na wananchi kwa ujumla.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati ya moyo wangu, ninakiri kuwa uongozi wake unaendelea kuwa chachu ya matumaini kwa Watanzania wote. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumtakia afya njema, hekima na maono makubwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza taifa letu.

**4.** Kadhalika, niungane na wewe, Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla, kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Deogratius John Ndejembi kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na kuthibitishwa na Bunge lako tukufu. Ninaamini uzoefu, weledi na uzalendo wake vitakuwa chachu muhimu katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuliongoza Taifa letu na kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya Serikali kwa manufaa ya Watanzania wote.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza na kumtakia kila la heri Mheshimiwa Dkt. Deogratius John Ndejembi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika majukumu yake mapya. Mungu ampe hekima, afya njema na nguvu katika kulitumikia taifa letu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuendelea kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Tunazidi kumuombea heri na busara anapoendelea kutekeleza majukumu yake. Hakika, uongozi wake thabiti umejidhihirisha kwa vitendo kutokana na mapinduzi makubwa ya kiuchumi na kimaendeleo yaliyofanyika Zanzibar. Hakika, mkasi unaongea.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba pia nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa ufanisi. Katika kipindi chote cha Mkutano huu wa Nne, tumewaona mkiongoza mijadala kwa umahiri mkubwa. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati za Bunge ambao wamekuwa chachu katika kufanikisha shughuli za Bunge.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama unavyojua, kazi zote zinazokuja hapa Bungeni hupitiwa na Kamati za Bunge. Ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na Kamati zote za Bunge kwa kazi nzuri na michango yenye dhamira ya dhati ya kuboresha mipango na kazi zinazokusudiwa kutekelezwa na Serikali. Michango na maoni yenu yanaendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali. Hakika, hili ni Bunge la wananchi wa Tanzania na ni Bunge lililotumwa na wananchi na linalowafanyia kazi Watanzania waliowachagua.

**Uteuzi wa Viongozi**

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** tangu tulipohitimisha Mkutano wa Tatu wa Bunge la 13, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya uteuzi mbalimbali, ikiwemo uteuzi wa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Wenyeviti wa Bodi mbalimbali pamoja na Mabalozi. Nitumie fursa hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na kuwatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao mapya.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwakumbushe viongozi wote walioteuliwa kwamba katika utekelezaji wa majukumu yao wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo, sera na vipaumbele vya Serikali. Pia, kuweka juhudi na jitihada katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Pole kwa Waathirika wa Ajali na Matukio Mbalimbali**

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki, pamoja na wengine waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Ninamuomba Mungu awape subira waliopoteza ndugu zao, majeruhi wapone kwa haraka, na marehemu wote awape pumziko la amani.

## 2.0 SHUGHULI ZA BUNGE

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** leo tunapohitimisha shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge la 13, tumefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali, ikiwemo wajibu wa msingi wa kutunga sheria, kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria ya Serikali, pamoja na kujadili na kutoa maazimio mbalimbali. Katika Mkutano huu, yaliulizwa na kujibiwa maswali ya msingi 121, maswali ya nyongeza 351, pamoja na maswali 12 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

**Miswada**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Miswada, Bunge lako Tukufu limepokea na kujadili miswada mitano ambayo ilisomwa katika hatua mbalimbali:

**Mosi:** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 [*The Agricultural (Amendments) Bill, 2026*], umesomwa kwa hatua zake zote;

**Pili:** Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026, umesomwa kwa hatua zake zote;

| | |
|---|---|
| **Tatu:** | Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026, umesomwa kwa hatua zake zote; |
| **Nne:** | Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2026 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill*, 2026], umesomwa kwa hatua zake zote; na |
| **Tano:** | Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill*, 2026] umesomwa kwa hatua zake zote. |

**Azimio la Bunge**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa maazimio, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 na kwa kuzingatia wajibu wa Bunge, Bunge lako tukufu lilipokea na kujadili azimio moja kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani. Ninalipongeza Bunge lako Tukufu kwa kupitisha azimio hilo, na Serikali ipo tayari kwa utekelezaji wake.

**Taarifa ya Kamati**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa upande wa taarifa za Kamati, kupitia mkutano huu, Bunge lako tukufu limepokea na kujadili taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Ninalihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Serikali itafanyia kazi mapendekezo yote ya Kamati na itawasilisha Bungeni taarifa ya utekelezaji wake.

**Hoja ya Serikali ya Bunge Kumthibitisha wa Makamu wa Rais**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka tarehe 28 Agosti, 2026 nilitoa hoja ya kuliomba Bunge lako tukufu limthibitishe Mheshimiwa Dkt. Deogratius John Ndejembi kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Ibara ya 54 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine, ninampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuthibitishwa na Bunge lako tukufu kwa kishindo, jambo linaloonyesha imani ya Waheshimiwa Wabunge kwake na kwa Mheshimiwa Rais. Mimi pamoja na Mawaziri tuko tayari kuhakikisha kwamba tunatekeleza maelekezo yake, kutoa mrejesho wa kazi tutakazotekeleza na kumshauri kwa hekima.

**Miradi ya kimkakati na reli ya SGR**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama utakumbuka, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akilihutubia Bunge lako tukufu alibainisha dhamira yake ya dhati ya kukamilisha miradi yote ya kimkakati. Dhamira hiyo imedhihirishwa kwa kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya kielelezo iliyotekelezwa hapa nchini.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mmojawapo ambao umekamilika ni Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, kama ambavyo umeshuhudia. Katika

falsafa yake ya "*continuity and change*", sambamba na kukamilisha Bwawa la Julius Nyerere, Mheshimiwa Rais ana dhamira ya kukamilisha miradi ya kimkakati ya ujenzi, ikiwemo ujenzi wa SGR kwa vipande vyote.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tumeshuhudia hivi karibuni akizindua kipande cha Tabora–Kigoma. Ili kufanikisha azma hiyo, ninaielekeza Wizara ya Uchukuzi, kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania, iweke mkakati mahususi wa kuendeleza utekelezaji wa miradi hiyo kwa kasi. Na kwa umahususi, vipande vya Mwanza–Isaka, Isaka–Tabora, Tabora–Kigoma na Makutupora–Dodoma.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipande cha Isaka–Mwanza kiko katika hatua nzuri na huenda kuanzia sasa hadi Desemba kikawa katika hatua ya ukamilishaji. Tutabaki na vipande vya Isaka–Tabora na Makutupora–Tabora ambavyo navyo viko katika hatua za utekelezaji.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaziagiza Wizara ya Fedha na Wizara ya Uchukuzi, zikishirikiana na Shirika la Reli, wakandarasi waliopewa kazi ya kujenga vipande hivi pamoja na wale waliopewa jukumu la kuhamasisha fedha za miradi hiyo, kupambana usiku na mchana. Ikiwezekana, ifikapo mwaka 2030, wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka Mwanza, Mara, Shinyanga, Geita, Kagera, Rukwa, Katavi na Kigoma wanaweza, kwa kuanzia, kuikamata reli pale Tabora waje Dodoma wakiwa wamepanda SGR. Kwa uzoefu tulioupata kwenye vipande vingine na katika ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere, hili ni jambo linalowezekana.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kuandaa utaratibu wa utekelezaji wake, nitakutana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi, wakandarasi pamoja na wale tuliowapa jukumu la kuhamasisha fedha za miradi hiyo. Tukimbie ili mradi huu uweze kukamilika na kufungua uchumi wa nchi yetu.

**Mradi wa Julius Nyerere wa kuzalisha umeme**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote ni mashahidi, na wengi wetu, hasa Waheshimiwa Wabunge, tulihudhuria na kushuhudia hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Kufua Umeme cha Julius Nyerere, iliyofanyika tarehe 22 Agosti, 2026 na kuongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nirejee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kujitoa na kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele katika kukamilisha utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu si wa kuzalisha umeme pekee, bali umeitambulisha Tanzania kwamba ni nchi inayoweza kusimamia maazimio yake, mipango yake na kutimiza mipango iliyojiwekea. Leo tunapozungumzia kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere, tunayo mambo mengi ya kujivunia.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kituo hiki si cha kuzalisha umeme tu, bali ni mfumo mzima wa miundombinu unaohitajika ili kuzalisha umeme jumla ya megawati 2,115. Uzalishaji huo umeongeza kwa kiwango kikubwa uwezo wa Taifa wa kuzalisha umeme na kuimarisha uwezo wa Gridi ya Taifa kusafirisha umeme na kuupeleka kwenye Gridi ya Taifa. Ndiyo maana mikoa ambayo haikuwahi kuwa kwenye Gridi ya Taifa sasa inaingia kwenye Gridi kukidhi mahitaji yanayotokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye aliipokea nchi ikiwa mradi huu ulikuwa umekamilika kwa takribani asilimia 33, sambamba na miradi mingine mikubwa. Jambo hili lingeweza kukatisha tamaa kutokana na ukubwa wa mradi, lakini hakuyumba na mpaka sasa miradi hiyo imeweza kukamilika.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** kituo hiki cha kuzalisha umeme, kwa uendelevu kinategemea upatikanaji wa maji ya uhakika. Kwa msingi huo, nazielekeza Wizara pamoja na mikoa husika kushirikiana katika kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya kuhifadhi mazingira, vyanzo vya maji na matumizi endelevu ya rasilimali katika Bonde la Rufiji, pamoja na vyanzo vingine vinavyopeleka maji kwenye Bwawa la Julius Nyerere.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hatua hiyo, Wizara ya Nishati iendelee kutekeleza mpango wa kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia mchanganyiko wa vyanzo mbalimbali vya nishati. Vyanzo hivyo ni ikiwemo maji, gesi asilia, jua, upepo, jotoardhi, makaa ya mawe na vyanzo vingine.

**Bima ya Afya Kwa Wote**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kulielezea Bunge lako tukufu kuhusu mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, ambao pia Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiulizia. Serikali imeanza kutekeleza mpango huu tangu Januari, 2026. Nawaomba Watanzania wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge tutofautishe Bima ya Afya kwa Wote na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, yaani TASAF. Bima ya Afya kwa Wote si mpango wa TASAF wala si mfuko wa TASAF.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** serikali kwa sasa inasaidia makundi ambayo hayawezi kumudu kuchangia Bima ya Afya kwa Wote. Lakini ili mpango huu uweze kutekelezeka, ni lazima Watanzania wote waingie kwenye mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote. Ninawakumbusha Watanzania kwamba bima hii si sawa na TASAF. Bima ya afya ni mpango unaomtaka kila Mtanzania mwenye uwezo kujiunga ili kupitia mfumo huo tuweze kuwasaidia wale wasio na uwezo.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninakumbuka kauli ya Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Yahya Nawanda alipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Iramba, ambapo alikuwa akitumia kauli ya "Jogoo mmoja, matibabu mwaka mzima." Maana yake ni kwamba kila Mtanzania atumie sehemu ya kipato chake kuunga mkono Bima ya Afya ili tuweze kuwasaidia wale wasio na kipato.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadiri Watanzania watakavyohamasika kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote, ndivyo mfumo wetu wa bima utakavyokuwa na ufanisi mkubwa na kuweza kuwasaidia Watanzania wenye mahitaji. Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari imeweka zaidi ya shilingi bilioni 48 na inaendelea kusaidia matibabu ya magonjwa ambayo Watanzania wengi hawawezi kumudu gharama zake. Twende kwenye Bima ya Afya ili tuwasaidie Watanzania wote.

**Sekta ya Madini**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya madini imeendelea kuwa nguzo kuu ya uchumi wa taifa letu na ni miongoni mwa sekta zinazoongoza katika kuchangia pato la Taifa.

Nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Madini inayoongozwa na ndugu yetu Anthony Mavunde kwa kusimamia vyema maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufanya mageuzi katika sekta hii.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio katika sekta ya madini yametokana pia na mchango mkubwa wa wadau wa madini. Kipekee, ninawapongeza wadau wote wa sekta ya madini kwa mchango wao katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya wachimbaji wakubwa, mchango wa wachimbaji wadogo katika uzalishaji wa madini umeendelea kuongezeka siku hadi siku. Hii imetokana na kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuweka mazingira wezeshi kwa Watanzania kunufaika na sekta hiyo. Hata hivyo, Serikali inatambua kuwa bado zipo changamoto mbalimbali ambazo tumeendelea kushauriana na Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa changamoto hizo ni tozo zinazowakabili wachimbaji wa madini na tozo nyingine katika maeneo ya halmashauri ambazo ziko juu ya kiwango kilichoainishwa katika sheria. Kwa mujibu wa sheria, tozo hizo zinapaswa kuzingatia kiwango kilichowekwa kisheria. Kuanzisha tozo zaidi ya kiwango hicho ni ukiukwaji wa sheria. Ninaiagiza Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, wakae kwa haraka na kuangalia changamoto hizo ili kuhakikisha ufanisi endelevu unaopatikana katika sekta ya madini unaendelea.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninazo taarifa kwamba katika baadhi ya maeneo kuna watu wanaoshikilia leseni nyingi kwa muda mrefu bila kuziendeleza, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya sheria ya madini. Maeneo makubwa ya uchimbaji na leseni nyingi zikishikiliwa na mtu mmoja bila kuendelezwa, husababisha Watanzania wengine kukosa nafasi ya kufanya shughuli za uchimbaji, hasa wachimbaji wadogo.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutatua changamoto hiyo, naiagiza Wizara ya Madini ichukue hatua za haraka na kali kwa mujibu wa sheria. Hatua hizo ni pamoja na kufuta leseni ambazo zimeshikiliwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa na kuyagawa upya maeneo hayo kwa Watanzania, hususan vijana na wachimbaji wadogo wanaohitaji maeneo ya kufanya shughuli za uchimbaji.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** yeyote anayetaka leseni yake isifutwe lazima atimize masharti yaliyowekwa katika leseni yake na kuiendeleza. Hatua hizi zichukuliwe kwa wale watakaokiuka sheria. Mheshimiwa Waziri, futeni leseni hizo kwa mujibu wa sheria na gaweni upya maeneo hayo kwa wawekezaji Watanzania, vijana wa Kitanzania na wachimbaji wadogo.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** haya ni miongoni mwa hatua ambazo Mheshimiwa Rais ameshazichukua katika maeneo mbalimbali kwa kufuta leseni na kuwawezesha vijana wa Kitanzania kufanya shughuli za uchimbaji. Hatua hizo zimechangia kuongeza mapato na uchumi wa vijana wa Kitanzania.

**Tahadhari ya mvua na El Niño**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na hayo, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imetoa utabiri wa mwelekeo wa mvua za msimu wa vuli kwa mwaka 2026 kuanzia mwishoni mwa Septemba, Oktoba hadi Desemba. Utabiri huo umebainisha uwepo wa hali ya El Niño ambayo itaambatana na mvua kubwa.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** mvua za vuli zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya Ukanda wa Pwani Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini, Mashariki, Ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya Septemba na wiki ya kwanza ya Oktoba katika maeneo yaliyotajwa. Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kuambatana na mafuriko na kusababisha madhara makubwa kiafya, kiuchumi na kijamii, pamoja na upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** serikali inaendelea kuchukua hatua za tahadhari na kutoa maelekezo katika maeneo mbalimbali ili kuimarisha maandalizi na kukabiliana na madhara yanayoweza kusababishwa na mafuriko. Hatua hizo ni pamoja na:

**Moja:** Kuimarisha Kamati za Maafa ili ziweze kukabiliana na madhara yanapojitokeza, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya miundombinu na kuirejesha katika hali ya kawaida;

**Mbili:** Nimezielekeza mamlaka husika kuchukua hatua stahiki ili kuzuia au kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza;

**Tatu:** Ninaziagiza Kamati za Maafa katika ngazi mbalimbali, kuanzia vijiji hadi Taifa, kujipanga kikamilifu kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza;

**Nne:** Maeneo yote hatarishi yatambuliwe mapema, tathmini za vihatarishi zifanyike na hatua stahiki zichukuliwe;

**Tano:** Tuhakikishe vifaa vya uokoaji, huduma za dharura pamoja na mifumo ya mawasiliano vinakuwa katika hali ya utayari;

**Sita:** Idara na taasisi zinazohusika na miundombinu na usafi wa mazingira zihakikishe barabara zinapitika wakati wote, mitaro na makalavati yanaimarishwa na kusafishwa ili kuzuia mifereji kuziba na kusababisha hata mvua za kawaida kuleta madhara;

**Saba:** Kwa upande wa sekta ya maji, umeme na mawasiliano, nazo ziweke mipango ya kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza ili huduma hizo ziwe endelevu; na

**Nane:** Aidha, tunazo mashine za kuchimba mabwawa. Zitumiwe kuweka miundombinu ya kudhibiti mafuriko katika maeneo ambayo maji yanatapakaa kwa sababu hayana pa kwenda.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie Bunge lako tukufu kuwakumbusha wananchi wa Tanzania kwamba taarifa za utabiri wa hali ya hewa zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ni taarifa muhimu na zitumike kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

**Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa lengo la kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji na kupunguza umaskini nchini. Katika kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu

katika shughuli za kiuchumi na kuwa na uwezo wa kujitegemea kiuchumi, Serikali imechukua hatua mbalimbali, ikiwemo:

**Moja:** Kuimarisha usimamizi na uratibu wa mifuko ya uwezeshaji;
**Mbili:** Kuratibu na kusimamia uwezeshaji wa wananchi kupitia vituo vya uwezeshaji;
**Tatu:** Kuratibu na kusimamia masuala ya uendeshaji wa biashara nchini; na
**Nne:** Kuweka utaratibu wa kutenga asilimia 30 ya zabuni za Serikali kwa ajili ya makundi maalum kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kama sheria inavyoelekeza.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** jana tarehe 03 Septemba, 2026 nilizindua kongamano la kuwawezesha Watanzania kushiriki katika shughuli za kiuchumi, uwekezaji na miradi ya kimkakati, ili tuweze kujenga sekta binafsi inayomilikiwa na Watanzania na hivyo kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wa Kitanzania na kuongeza mapato ya nchi yetu. Serikali pia imeendelea kutekeleza suala la mikopo kwa vijana pamoja na mikakati ya urejeshaji.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa Wizara na taasisi zinazohusika kuendelea kulitekeleza jambo hili kikamilifu na kwa ufanisi, ili fedha zaidi ya shilingi bilioni 200 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais ziweze kuwafikia Watanzania wanaohusika, hususan vijana, wanawake na makundi maalum.

## 3.0 MAELEKEZO MAHSUSI

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** nikiwa naelekea kumaliza, naomba nitumie fursa hii kutoa maelekezo mahususi. Katika ziara zangu mbalimbali nilizofanya mikoani, nimeona, kama ilivyokuwa katika ziara za Mheshimiwa Rais katika mikoa mbalimbali, kwamba wananchi wengi wana masuala yanayowagusa moja kwa moja. Masuala hayo ni pamoja na upatikanaji wa huduma za jamii, utatuzi wa migogoro, utatuzi wa kero za wananchi kwa wakati na kutoa mrejesho wa hoja zinazowasilishwa katika ofisi za umma.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatumia fursa hii kusisitiza kwa Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, watendaji wote wa Serikali na watendaji wa halmashauri tufanye kwa vitendo na kutoa mrejesho pale tunapotatua kero za wananchi. Ziara za Viongozi Wakuu zisiwe mbadala wa utatuzi wa kero na utekelezaji wa shughuli za kila siku za Serikali.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini iliyofanyika imebaini kuwa, wananchi wengi wameendelea kuwasilisha kero zao moja kwa moja kwa viongozi wa kitaifa. Huu si utaratibu wa kawaida. Tuna ofisi za Serikali mpaka ngazi ya vitongoji na mitaa. Haipaswi mwananchi wa kawaida ahangaike kupeleka kero yake mpaka mkoani au kitaifa wakati kuna mnyororo wa utendaji wa Serikali katika kila eneo.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa msingi huo, nawaagiza tena watendaji wote wa Serikali, waweke utaratibu wa kuwasikiliza wananchi, kutatua kero zao na kutoa mrejesho. Kwa kero ambazo haziwezi kutatuliwa katika ngazi husika, watendaji wa Serikali wenyewe wazipeleke katika ngazi zinazofuata kwa ajili ya utatuzi.

**Utekelezaji wa Vipaumbele vya Bajeti**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawaagiza watendaji wa Serikali waendelee kuzingatia kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa katika bajeti zetu. Lengo ni kujenga uchumi imara na himilivu kupitia mageuzi ya kidijitali, uwekezaji na utekelezaji wa mikakati na sera endelevu za kibajeti ili kukuza uchumi.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele hivyo, kama vilivyoainishwa na Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, ni pamoja na utawala, amani na usalama; uchumi imara na shindani; uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii; uhifadhi wa mazingira; pamoja na sekta za vichocheo vya kimageuzi.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni jukumu la kila mtendaji kuhakikisha fedha zinazotengwa zinatekelezwa na kuelekezwa katika miradi husika kwa wakati na kuleta tija. Ninasisitiza ubora wa miradi uendane na thamani halisi ya fedha (value for money). Katika kutekeleza vipaumbele hivi, Waziri wa Fedha alitoa rai ya kubana matumizi na kuelekeza fedha katika vipaumbele.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia hilo, nazielekeza taasisi za Serikali zichukue hatua katika maeneo ambayo matumizi yanaweza kupunguzwa bila kuathiri ufanisi wa shughuli za Serikali. Maeneo hayo ni pamoja na:

a) Matumizi ya uendeshaji wa magari ya Serikali;
b) Matumizi ya shajara;
c) Gharama za safari za ndani na nje;
d) Gharama za michakato ya bajeti;
e) Idadi ya watumishi wanaoshiriki katika michakato hiyo;
f) Gharama za mikutano;
g) Warsha na makongamano; na
h) Safari nyingine zisizo za lazima.

Kwa hiyo, haya ni baadhi ya maeneo ambayo tunaweza kuyarekebisha bila kuathiri shughuli za Serikali.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** bado tuna fursa kubwa ya kupunguza matumizi haya. Ninayo mifano, nilipokuwa mbunge, nakumbuka nimewahi kuwa mjumbe wa Kamati ya Bunge ya LAAC. Inapofika wakati wa kujadili bajeti ya TAMISEMI, Wakurugenzi na CMT inaweza kuwa na watu takribani 14 wanakuja Dodoma kutoka nchi nzima.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukiongeza wakurugenzi na watendaji wengine wa mkoa, mkoa mmoja unaweza kuja na watu 100 hadi 180. Kwa nchi nzima, inaweza kuwa watu 5,500 hadi 6,000. Lakini katika chumba cha Kamati ya Bunge, wanaozungumza mara nyingi ni watu watatu au wanne tu. Wengine wote husubiri nje. Haya ni mambo ya mazoea ambayo tunaweza kuyaepuka na fedha hizo tukazipeleka katika ujenzi wa madarasa ambayo yatahitajika sana tunapoanza kutekeleza mageuzi mapya ya elimu.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimeshuhudia pia katika ziara kwamba haya ni mambo ya mazoea. Unaenda mkoa fulani ambako unatarajia kutembelea wilaya zote, lakini watendaji wa mkoa mzima, pamoja na watendaji wa wilaya nyingine, wote

wanaenda katika wilaya unayotembelea. Matokeo yake, mnakwenda kukagua darasa lililojengwa kwa shilingi milioni 24 mkiwa na magari 150, na gari la mbunge linakuwa la 151.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninamuelekeza Waziri wa TAMISEMI, awaelekeze Wakuu wa Mikoa na idara mbalimbali kwamba haya ni mambo tunayoweza kuyaepuka. Wanaweza kwenda kujadili bajeti na kumaliza masuala hayo huko huko mikoani. Afisa Masuuli ambaye ni Katibu Tawala wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa na Afisa Bajeti wanaweza kwenda kukutana na Kamati ya Bunge.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nini tunapokwenda kukutana na watu wa IMF au Benki ya Dunia tunawakuta watu wawili tu, wakati upande wetu tuna watu 50? Ukienda kukutana na Balozi, utakutana na Balozi pamoja na msaidizi wake, wakati upande wetu watu wanaweza kuwa zaidi ya 30. Haya ni mambo ya mazoea.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** kila Katibu Tawala wa Mkoa aisome na kuielewa bajeti ya mkoa wake. Mkuu wa Mkoa afungue kikao na awakaribishe wataalamu waliotoka mkoani kwake. Katibu Tawala na Afisa Bajeti wazisome na kuzielewa bajeti hizo. Utaratibu wa kuleta watendaji wote jijini Dodoma unapaswa kupunguzwa.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** halmashauri zipo zaidi ya 180. Kama kila halmashauri inakuja na magari matatu, tunapata zaidi ya magari 500, ambayo yanatumia mafuta. Mkutano mmoja wa kujadili bajeti ambapo wanaozungumza ni watu wachache unaweza kutumia zaidi ya shilingi bilioni 20. Tunahitaji fedha hizo kujenga madarasa tunayohitaji ili kukamilisha mageuzi katika elimu.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia mwaka 2028, tunatarajia watoto wanaoanza Kidato cha Kwanza watakuwa mara tatu ya idadi ya wanaoanza Kidato cha Kwanza kila mwaka. Hapo awali, walikuwa wanaanza takribani 900,000, lakini katika kipindi hicho wanatarajiwa kuwa zaidi ya milioni tatu.

***65.*** ***Mheshimiwa Spika,*** tutahitaji zaidi ya vyumba 8,000 vya maabara, zaidi ya vyumba 16,000 vya madarasa, pamoja na zaidi ya walimu 27,000. Lazima tubadili tabia ya matumizi. Tusipobadili tabia ya matumizi, watoto wetu wanaweza kurudi tena kusomea chini ya miti. ***Tusirudi huko. Tayari tumeshavuka.***

**Tozo katika Serikali za Mitaa**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, tunazo tozo mbalimbali katika halmashauri na Serikali za Mitaa kwenye uzalishaji wa mazao, yakiwemo madini, mifugo na kilimo. Maelekezo yangu hayana tofauti na yale ya awali: tuzingatie sheria. Sheria inataka kwamba kama tunataka kuanzisha tozo mpya, tusipitishe kabla ya kushirikisha Wizara ya Fedha, ili kuepuka kuanzisha tozo juu ya tozo nyingine na kuwapa mzigo mkubwa wananchi pamoja na wazalishaji.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninalishukuru Bunge lako tukufu kwa kuridhia na kupitisha marekebisho yaliyokuwa yanapendekezwa katika baadhi ya maeneo yaliyolenga kuleta ufanisi. Tumebadilisha namna ya kuoanisha muda wa uongozi baina ya Meya na Naibu Meya sambamba na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ili kuimarisha uwajibikaji katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** sasa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, Meya na Naibu Meya watakuwa na muda wa uongozi wa miaka mitano, ili kuondoa fujo za watu kupanga makundi kila wakati na kuacha shughuli za kuwatumikia wananchi.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** tuna utaratibu wa kumwajibisha yule anayefeli. Kwa nini tutumie kigezo kwamba tunaweza kuchagua mtu asiyefaa? Tukichagua mtu asiyefaa, tumtoe. Lakini tusifanye nchi nzima iwe kwenye uchaguzi kila mwaka. **Ninalipongeza sana Bunge lako kukubali pendekezo hili la Serikali.**

**Kalenda ya Vikao vya Halmashauri**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuna jambo moja ambalo tulishalisema, na hapa nimwelekeze Waziri wa TAMISEMI. Kwa kuwa ratiba za Bunge zinafahamika, kila mara tunalalamika kwamba Waheshimiwa Wabunge wanakosa vikao vya halmashauri. Kwa kuwa ratiba ya Bunge inafahamika, hata hapa kabla ya kutoa hoja, ninataja kwamba kikao rasmi cha Bunge lijalo kitakuwa na tarehe yake.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumwelekeza Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI aandae kalenda ya vikao vyote vya madiwani na kuvifanya wiki tatu kabla ya tarehe rasmi ya kuanza kwa Bunge. Wiki tatu kabla ya kuanza Bunge, maana yake ni wiki moja kabla ya Kamati za Bunge kuanza kukutana. Kwa hiyo, vikao hivi vifanyike kabla ya Kamati za Bunge kuanza kukaa.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo ni kuwapa fursa Waheshimiwa Wabunge ambao kisheria ni madiwani kushiriki vikao hivyo kabla kuja katika shughuli za Bunge. Ni wazi kuwa yapo maeneo ambayo wabunge wanakoseshwa vikao hivyo kwa makusudi. Hii si siri, na siwasemi wote; nawalenga wale wenye tabia hizo.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama kuna Mkurugenzi ambaye tayari ana kundi lake pale, wanaweza kupanga vikao ambavyo kwa vyovyote vile Mbunge atakosa. Lakini tumeweka katika sheria kwamba Wabunge ni madiwani, kwa hiyo sheria lazima itekelezwe. Kama tunaona Wabunge si muhimu katika vikao vya madiwani, tubadilishe sheria. Lakini tusiwe na sheria inayowataka Wabunge kushiriki halafu hawashirikishwi ratiba. Kwa kuwa tumeshazungumzia jambo hili na tulitoa tamko wakati Bunge likiendelea, kuanzia sasa atakayekiuka ni mkaidi na hastahili kuwa katika ofisi hiyo.

## 4.0 MICHEZO

**Maandalizi ya AFCON 2027**

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimalizie kwa upande wa michezo. Serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya AFCON 2027. Nitumie nafasi hii kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba kazi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu inaendelea kwa kasi kubwa. Miundombinu hiyo ni pamoja na viwanja vya mazoezi, viwanja vya mashindano, barabara za kuingia na kutoka viwanjani, pamoja na huduma za afya, maji, umeme na miundombinu mingine wezeshi.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa viwanja, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa uwanja wa Jiji la Arusha, ambao umefikia zaidi ya asilimia 91,

pamoja na ujenzi wa uwanja wenye uwezo wa kuchukua zaidi ya watazamaji 32,000. Kwa upande wa Zanzibar, Uwanja wa Fumba nao uko katika hatua nzuri.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Dar es Salaam, ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa pamoja na viwanja vya mazoezi vya Gymkhana, Meja Jenerali Isamuyo na Shule ya Sheria tayari umekamilika. Kwa upande wa Zanzibar, mbali na uwanja wa Fumba, kuna pia New Amani Complex Annex 1 na Annex 2, ambavyo vimekamilika, pamoja na uwanja wa Amani ambao nao uko katika hali nzuri.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa wasimamizi wa miradi, nisisitize kwamba thamani ya fedha (*value for money*) ionekane katika miradi hiyo. Kutokana na umuhimu wa AFCON kiuchumi, nazielekeza Wizara na taasisi zinazohusika ziendelee kuratibu namna ambayo Tanzania itanufaika kwa kuwa mwenyeji wa mashindano haya. Wadau wote wahakikishe wanashiriki na pasiwe na mkwamo ambao utapunguza ufanisi au manufaa ambayo Tanzania ingeweza kupata kutokana na kuwa mwenyeji.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** sisi ni wenyeji wa mashindano. Tunapenda pia kuona timu yetu ya Taifa ikiwa na ubora na siyo msindikizaji. Nitoe wito kwa makocha pamoja na Shirikisho na benchi la ufundi wafanye jitihada kuhakikisha kwamba kuanzia sasa tunaweka mikakati madhubuti itakayowezesha timu yetu kufanya vizuri.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** najua wikiendi hii, timu zetu za ngazi ya vilabu zinaanza safari zao katika mashindano ya CAF. Simba, Yanga, Azam na Singida ni wawakilishi wa nchi yetu. Nitumie jukwaa hili la Bunge lako tukufu kuzitakia kila la heri timu zetu na kuwaomba Watanzania kwamba katika mashindano ya kimataifa tuache ushabiki wetu wa kawaida na tutangulize bendera ya Taifa.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** tuziunge mkono timu zote zinazoshiriki mashindano ya kimataifa ili ziweze kufanya vizuri. Inapofika kwenye mashindano ya kimataifa, mimi ni shabiki wa Simba na huwa napenda wanavyofanya. Nitoe wito hata kwako Mheshimiwa Spika, ni vema ukashabikia timu nyingine, ili tujenge uzalendo wa kuziunga mkono timu zetu zote za Tanzania.

## 5.0 SHUKRANI

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye amefanya kazi nzuri sana ya kutusaidia Wizara zote usiku na mchana, pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye amefanya kazi nzuri ya kuratibu na kusaidia shughuli hizi zinazokuja humu Bungeni. Ninawashukuru pia Wakuu wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, Mkuu wa Mhimili wa Mahakama na taasisi nyingine zote ambazo tumekuwa nazo bega kwa bega katika kumsaidia Mheshimiwa Rais.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, nimpongeze Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Idelphonce Leonard, pamoja na wasaidizi wake wote na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri na msaada mkubwa wanaotupatia katika kipindi chote tunapokuwa hapa Bungeni. Nirudie tena kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Said Johari. Amekuwa mwepesi sana pale Wizara na Idara za Serikali zinapokuwa na jambo linalohitaji ushauri wa Serikali. Tunamshukuru sana.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** nirejee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Hoja zenu zote mlizozitoa tutaendelea kuzifanyia kazi ili kuhakikisha yale ambayo wananchi wa Tanzania waliwatuma yanapata matokeo yake.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kumalizia, naendelea kuwaomba wananchi wa Tanzania kuendelea kuungana na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhimiza umuhimu wa amani, ushirikiano na umoja wetu wa kitaifa. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais amesema mara kadhaa, bila amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa, mipango yote tunayoiandaa, iwe ya Serikali, sekta binafsi au ya mtu mmoja mmoja, haiwezi kufanikiwa.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** jambo hili si la Serikali pekee; ni jambo la nchi nzima na ni jukumu la kila Mtanzania. Tuungane pamoja na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa ya amani, umoja, mshikamano na utulivu ili tuweze kutekeleza mipango yetu ya maendeleo. Nchi yetu inapiga hatua kubwa, na moja ya siri ya mafanikio hayo ni amani na utulivu.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru pia viongozi wote wa sekta binafsi pamoja na viongozi wote wa dini ambao wamekuwa nasi bega kwa bega katika shughuli za maendeleo. Sekta binafsi ni chachu kubwa ya maendeleo, na viongozi wa dini ni sehemu muhimu ya wadau tunaoshirikiana nao kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusonga mbele.

**Hoja ya Kuahirisha Bunge**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, sasa napenda kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liahirishwe hadi **Jumanne, tarehe 27 Oktoba 2026, saa 3:00 asubuhi**, litakapokutana tena hapa katika ukumbi wa Bunge jijini Dodoma.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.